

MIONGOZO YA SERA YA JERAHA LA KICHWA



Uondolewaji wa Wanafunzi Walioumia

Jeraha la ubongo litokanalo na mtikisiko mkali ndiyo aina kuu ya jeraha hatari la kichwa ambalo hutatiza utenda kazi wa kawaida wa ubongo. Hutokea pale ambapo ubongo unagonganishwa mbele na nyuma au kupinduliwa kwenye fuvu la kichwa kufuatia pigo kubwa kwenye kichwa au mwili. **Mwanafunzi yeyote anayedhaniwa kuwa amejeruhiwa ubongo kufuatia mtikisiko mkali au jeraha hatari la kichwa ataondolewa mara moja kutoka kwa shughuli yoyote, ikiwa ni pamoja na, na wala sio tu matukio ya michezo, kwa sababu sharti hilo lemefasiliwa chini ya sheria ya jimbo la Utah, ikiwemo michezo ya ndani ya darasa na baina ya shule, mazoezi, makambi ya michezo, mashindano, na majaribio ya michezo iliyokubaliwa na shule, michezo ya vilabu, ushangiliaji, densi, au shughuli zingine ambapo majeraha yanaweza kutokea. Shule itafuata kanuni ya kuwa: "Iwapo una shaka, usimhushishe mwanafunzi." Ili kupata taarifa kuhusu majeraha ya ubongo yanayosababishwa na mitikisiko mkali au majeraha mabaya ya kichwa, ikiwemo miongozo ya kudhibiti kwa saa 24 za kwanza baada ya jeraha, tazama kwenye kiungo cha UHSAA Sports Medicine, www.uhsaa.org/new/.**

Mwanafunzi au mchezaji atadhaniwa kuwa amejeruhiwa ubongo kufuatia mtikisiko mkali au ana jeraha mbaya la kichwa iwapo yoyote kati ya dalili zifuatazo zinaonekana au kuziripoti yeye mwenyewe baada ya kuumia kutokana na kugongwa, kusonga kwa ubongo kwenye fuvu kufuatia kugongwa kwa nguvu kwa kasi, au kuumia kwa ubongo kufuatia kusimama kwa ghafla kwa chombo kilichokuwa kikienda kwa kasi: (a) kupoteza fahamu ya wakati, kuchanganyikiwa, au hali ya kutoweza kufanya lolote ilhali unajifahamu; (b) kupoteza uwezo wa kukumbuka; (c) kupoteza fahamu; na/au (d) dalili za matatizo mengine ya kiakili au ya kiakili na ya kimwili ikiwemo: kifafa, kuudhika upesi, kukosa nguvu, kutapika, kuumwa na kichwa, kizunguzungu, na/au uchovu.

Dalili za kawaida na ushara ni pamoja na: (a) matatizo ya kumbukumbu ya muda (anasahau michezo); (b) matatizo ya kusimama bila kuyumbayumba au upatanifu; (c) majibu ya pole pole au yasiyo sahihi; (d) hali ya kuona vitu viwili viwili au mabadiliko katika hali ya kuona; (e) hali ya kudhuriwa na mwangaza au sauti/kelele; (f) kuzembea au kutokuwa wazi; (g) kukosa kuzingatia jambo kwa muda mrefu; (h) kutazama mahali bila kusita au ishara za uso zisizo wazi; (i) majibu yanayochelewa ya kuongea au ya kutenda (kujikokota katika kujibu maswali au kufuata maagizo); (j) kuchanganyikiwa au kutokuwa na uwezo wa kuzingatia jambo moja; (k) kukosa mwelekeo; (l) kuzungumza bila mpangilio au bila kueleweka; (m) hisia zisizowiana na hali halisi (kulia bila sababu yoyote); (n) upungufu wa kumbukumbu (kukosa uwezo wa kukumbuka maneno matatu au vitu vitatu ndani ya dakika tano); na/au (o) kipindi chochote cha kupoteza fahamu.

Uamuzi wa Kurudi kwa Mchezo

Uamuzi wa kurudi kwa mwanafunzi kwenye matukio ya michezo baada ya mtikisiko ya jeraha mbaya la kichwa ni uamuzi wa kimatibabu, na ni lazima mwanafunzi au mchezaji apata idhini inayofaa ya kimatibabu kabla ya kuruhusiwa kurudi kwenye mchezo katika tukio lolote la kimchezo. Wazazi wanahimizwa kuratibu hali ya mwanafunzi ya kurudi kwenye shughuli kamili na madaktari, wasimamizi wa michezo, wakufunzi, na wafanyakazi wengine wa shule. Hali ambazo zinaweza kuathiri hali ya kupona ya mwanafunzi au mchezaji ni pamoja na: kuwepo na hali ya mtikisiko hapo awali, muda na aina ya dalili, umri, na mchezo au shughuli ambayo mwanafunzi anashiriki. Mwanafunzi au mchezaji aliyewahi kupata jeraha moja au zaidi la ubongo linalosababishwa na mtikisiko mkali au majeraha mabaya ya kichwa, ambaye amekuwa na dalili za mtikisiko kwa muda mrefu, au ambaye anashiriki kwenye mchezo unaohusisha kugongana au kugusana anaweza kupona polepole.

Kabla ya mwanafunzi kurudi kwenye hali yake ya awali ya kushiriki kwenye mchezo, mwanafunzi huyo anapaswa kukaguliwa na mtoa huduma za afya ambaye ana leseni ya Jimbo la Utah na amepokea mafunzo katika kukagua na kudhibiti majeraha ya ubongo yanayosababishwa na mitikisiko mikali au majeraha mabaya ya kichwa. Ni lazima huyo mtoa huduma ya afya atoe akauli iliyoandikwa kwa shule akithibitisha kuwa, ndani ya miaka mitatu kabla ya siku ambayo kauli iliyoandikwa ilitolewa, amekamilisha kozi ya elimu ya kujiendeleza kitaaluma katika ukaguzi na udhibiti wa jeraha la ubongo linalosababishwa na mtikisiko mkali au jeraha mbaya la kichwa; na kwamba mwanafunzi anaruhusiwa kuendelea kushiriki katika mchezo fulani.

Mzazi au mlezi wa kisheria ni lazima atoe ruhusu iliyoandikwa kwa mwanafunzi huyo. Uamuzi wa kurudi kwenye shughuli za michezo hautaharakishwa ili kufaidi timu au kwa sababu nyingine yoyote. **Mfano wa utaratibu wa kurudi kwenye mchezo na fomu ya kumuidhinisha mwanafunzi inaweza kupatika katika ukurasa wa tovuti wa <http://www.graniteschools.org/curriculuminstruction/wp-content/uploads/sites/29/2015/01/Athletics-Concussion-Management-Plan.pdf>.** Sera kamili ya wilaya kuhusu jeraha la kichwa inaweza kupatikana katika <http://www.graniteschools.org/legal/wp-content/uploads/sites/22/2015/05/VIII.A.29.-Student-Head-Injuries-and-Concussions.pdf>



MIONGOZO YA SERA YA JERAHA LA KICHWA

Kipindi cha Mwaka wa Shule wa 2017 hadi 2018

Kwa kutia saina, ninakubali kuwa nimepitia na kuelewa taarifa zilizo kwenye Miongozo ya Sera ya Jeraha la Kichwa, na kwamba nimeshuriwa, kutahadharishwa, na kuonywa na Wilaya ya Granite hatari za majeraha yanayoweza kutokea kufuatia kushiriki katika shughuli za mazoezi ya mwili na michezo, kwa sababu sharti hilo limefasiliwa na sheria ya jimbo la Utah, na ambayo inajumuisha na wala sio tu darasa la mazoezi ya kimwili, darasa la elimu ya kawaida, wakati wa mapumziko au shughuli nyingine ambapo majeraha yanaweza kutokea. Nina ufahamu kamili kuwa kushiriki katika shughuli za mazoezi ya kimwili na michezo huweka wanafunzi kwenye hatari ya kupata majeraha madogo au mabaya, ikiwa ni pamoja na, na wala sio tu: mshtuko, kuvunjika kwa viungo, ulemavu wa mojawapo ya mguu au mkono au ulemavu wa miguu na mikono yote, jeraha kwenye ubongo, hali ya kupooza, na hata kifo. Ninaelewa kuwa maagizo ya mwalimu, vifaa vya kujilinda, na matibabu yanayotolewa havitoshi kumaliza hatari hizi. Nimeuliza maswali au kuwasilisha wasiwasi wowote nilio nao kwa walimu na maafisa wengine wa shule. Baadha ya kupata tahadhari na onyo, bado ningependa kumruhusu mwanafunzi aliyetajwa hapa juu kushiriki kwenye shughuli za mazoezi ya kimwili na michezo, na ninafanya hivyo nikiwa na ufahamu kamili wa hatari zilizopo.

Shule: _____

Jina la Mwanafunzi: _____ **Darasa la Mwanafunzi:** _____

Saina ya Mzazi au Mlezi: _____